

CONSTITUTION OF KENYA REVIEW COMMISSION

CKRC

VERBATIM REPORT OF

CONSTITUENCY PUBLIC HEARINGS

MASINGA CONSTITUENCY, PUBLIC HEARINGS

HELD AT MASINGA CATHOLIC CHURCH HALL ON

23RD MAY 2002

**CONSTITUENCY PUBLIC HEARINGS, MASINGA CONSTITUENCY, PUBLIC HEARINGS HELD AT
MASINGA CATHOLIC CHURCH , ON 23RD MAY 2002**

Commissioners Present

1. Com. Pastor Zablon Ayonga
2. Com. Mrs. Phoebe Asiyó

3. Com. Dr. Charles Maranga
4. Com. Mutakha Kangu

Secretariat Staff in Attendance

1. Mr. Peter Kanyi - Programme Officer
2. Lydia Manyoni - Assistant Programme Officer
3. Jackie Nyumoo - Verbatim Recorder
4. Rose Ngina Kimeu - District Co-ordinator

Meeting started at 9.30 a.m. with Com. Pastor Zablon Ayonga in the Chair.

Chairman of 3C's: Ningetaka tuanze mukutano wetu wa leo, na kwanza ningemuuliza Pastor Mulandi atufungulie Mukutano kwa maombi.

Prayer

Pastor Mulandi: Baba, katika jina la Yesu Christo Mwokozi wa maisha yetu, U-tegemeo letu . Na asubuhi ya leo Mwenyezi Mungu Baba umetuamusha na umetuleta hapa Masinga kwa ajili ya jambo ambalo nchi yetu ya Kenya tukufu, Mwenyezi Mungu Baba lina jambo la kuangalia na kutengeneza katiba.

Mwenyezi Mungu Baba watumishi wako Commissioners wameingia na tunakushukuru kwa kuwajalia na kuwaleta salama. Pia tunawaomba wale ambao ni wa constituency na wale ambao wameingia na wale ambao wanakuja, ili Mwenyezi Mungu Baba kutaniko letu hapa, liwe baraka kwako na maoni yote ambayo yatatolewa, Mwenyezi Mungu Baba ujalie watumishi wako Commissioners, wakiunganisha yote, Mwenyezi Mungu Baba baadaye, tuone mkono wako na kuona katiba ambayo itakuwa ikijali masilahi ya nchi yetu ya Kenya yote. Mwenyezi Mungu Baba asante kwa kila jambo. Kuwa pamoja na sisi, tumeanza pamoja na wewe, twaomba ili utuongoze, utubariki, na tukiona mwisho wa siku ya leo, hatutasahau kusema ni asante. Asante kwa kila jambo na ni katika jina la Yesu Christo Mwokozi wetu tunaomba, Amen.

Chairman of 3C's: Na sasa ningependa kuwajulisha members wa Constituency Committee, wenye wako hapa, na tafadhali wenye wamefika mukasimame Commissioners waweze kuwaona. Na members wa Constituency Committee, members wa Constituency Committee pekee yao. Na kwa upande wangu wa kulia, niko naye Mr. John Kasia, huyo ndiye Chairman wa Constituency Committee ya Masinga, na karibu na yeye kuna Pastor Mulandi. Pastor Mulandi is our Secretary wa the 3C's, na pale kuna Mrs. Jane Kilonzo, Jane Kilonzo pia ni member wa ile Constituency Committee ya Masinga. Shukurani.

Sasa tutawapatia Commissioners nafasi, nao tuweze kuwajua, na tukaweza kuanza Mukutano wetu wa leo, asanteni.

Com. Pastor Zablon Ayonga: Nataka, kabla hatujaanza, Commissioners kujijulisha kwenyu. Katika mkono wangu wa kulia mwisho,

Mimi ni Mama Phoebe Asiyo, Commissioner wa hii mambo ya kubadilisha katiba ya Kenya.

Com. Pastor Zablon Ayonga: Na karibu nami hapa mkono wa kulia bado;

Naitwa Dr. Charles Maranga, mimi ni Commissioner.

Com. Pastor Zablon Ayonga: Na mkono wangu wa kushoto, mwisho.

Mimi naitwa Mutakha Kangu, ni moja wa ma-Commissioners.

Com. Pastor Zablon Ayonga: Na mimi ni Pastor Zablon Ayonga, Commissioner. Sasa chukuwa microphone na tua majina yako - - - Na tutampa dakika tano za kuweza kutoa maoni yake. Inawezekana mtu amekuja, ana maandishi, memorandum. Na kama ana memorandum, tutataka atumulikiye maneno yale makubwa makubwa ambaye ametaka, hiyo itakuwa ni uchaguzi wake. Lakini asipotaka pia kufanya hivyo, anaweza kutoa memorandum yake pila kusema kitu chochote. Sisi tutaichukuwa hiyo memorandum pamoja nasi tukirudi Nairobi, na tutaenda kuisoma kuona maoni yake.

Mwingine anaweza kuwa ni yule ambaye anataka kutoa maoni yake ambayo hakuandika, verbal submission, na anaruhusa ya kufanya hivyo, na pia kama Commissioners watataka kumuuliza maswali watamuuliza, na kama hataulizwa maswali, atajiandikisha. Kila moja ambaye atatoa maoni lazima ajiandikishe. Tuna register hapo, utajiandikisha, utaweka sahihi kwamba umetoa maoni. Lakini kila wakati, ambao mtu ameitwa hapa mbele kwa kutoa maoni, tunataka utunze saa.

Leo si siku ya kutuuliza sisi maswali, leo ni siku yako kutuambia maoni, na unapo tuambia maoni, tunataka kusikia ni vitu gani unavyotaka vifanyike. Ni vitu gani unataka vibadilishwe? Na kama vinabadilishwa, unataka vibadilishwe namna gani? Si kwamba unasema sasa mwende muangalie hayo maneno. Tumefikiri na tumekupa time ya kujua kwamba by now, umejua ni nini unachokitaka, na kile unachokitaka ndiyo tunataka utuambie, tunataka hapa, hii ifanywe hivi na hivi, hayo ndiyo maoni.

Na lugha. Una uhuru wa kutumia lugha tatu. Tatu ikiwa hivi. Ikiwa umejitayarisha na maoni yako kwa kingereza utatupa maoni yako kwa kingereza. Ukiwa umejitayarisha na maoni yako kwa Kiswahili, utatupa maoni yako kwa Kiswahili. Ikiwa, umetayarisha maoni yako kwa lugha ya mama, utatoa maoni hayo kwa lugha ya mama. Na kwa hivyo una uhuru wa kufanya upendavyo kufuatana na uwezo wako ambao unaweza kutoa maoni yako. Kwa hiyo tungependa useme maneno yakiwa sawa sawa, maneno ambayo yamelinga yale ambaye yamewaleta hapa.

Kitu kingine, tuliwatumia kile kijitabu cha rangi ya uthurungi, ambacho ni Questions na mambo ya namna hiyo. Tafadhali hapa hatukuwaleta kama class room, ambayo leo utakuja hapa mbele, na kuanza kutuambia hivi.

Swali number moja, uliuliza hivi hivi hivi, jibu ni hivi, hivi, vile na vile. La! Kile kitabu kilikuwa kinakupa muongozo, wa kuchanga mtu katika mawazo yako uanze kufikiri kuna mambo ya namna hii, kuna mambo ya namna hii, na uanze kufikiri jinsi ambayo unaweza kutoa maoni yako. Kwa hivyo tafadhali msije kutujibu na hicho kitabu, kwa maana kama ni hicho kitabu ambacho kimetuleta hapa, ni mtu moja tu anaweza kuanza kutusomea hiyo maswali, na atupe majibu na maneno iishe. La! Si hivyo ingekuwa. Tungetaka mtupe maoni yenu ya namna zote ambayo inahusu uchumi wa nchi yetu, utawala wa nchi yetu, maisha tunayoishi, matumizi ya land, ardhi tuliyonayo, tungependa kuitumia namna gani? Mali tuliyo nayo. Vitu vya namna mbali mbali kwa maana kila moja anawazo lake. Na jinsi ya kuishi katika nyumba na vile na vile. Kwa hivyo niko tayari kuita majina, na ukiitwa jina, tafadhali unakuja unakaa hapa.

Basi tuko tayari na nitaanza kuita majina. Stephen Ndavi Muthembwa. Tafadhali uje mzee. Dakika tano. Stephen Muthembwa unapoanza unasema majina yako jinsi yalivyo ili yaiingie kwa kanda.

Stephen Ndavi Muthembwa: Bwana Commissioner, niliyaandika maoni ya kikundi changu. Mimi Naitwa Stephen Ndavi Muthembwa. Nimeleta maoni ya kikundi changu katika Sub-Location ya Kikumeni, na ndiyo mimi nataka kuwapea saa hii.

Com. Pastor Zablon Ayonga: Unaweza kumulika hayo mawazo au unataka kusoma?

Stephen Ndavi Muthembwa: Kusoma naweza soma nisome?

Com. Pastor Zablon Ayonga: Ah, Ah. Hatutaki utosomee, unaweza kutuambia maneno makubwa makubwa.

Stephen Ndavi Muthembwa: Kikundi changu kinaonelea katika muongozo wa serikali, kwanza utangulize tuwe na maombi. Tukianza kitu na kuheshimiana kwa kila mtu na kuheshimu mjadala tunao. Kama sisi tunajadiliana kitu, kuheshimu hiyo mpango. Na kuheshimu katiba ya Kenya, na Mwenyezi Mungu, na serikali yetu.

Haki za watoto wa Kenya ziheshimiwe. Kama inawezekana tuwe na elimu ya bure katika Kenya. Maoni mengine, iwe ni lazima Kanisa kuongoza sera ya dola. Iwe lazima President atawale katika miaka mitano, na asirudie tena. Na kwenye katiba, kanuni za democracia ziwe ni President, Vice President, Prime Minister, Mkuu wa Sheria na Mawaziri. Wakenya wana maadhili muhimu yanayo paswa kuwekwa kwenye katiba kama sheria za kitamaduni katika Kenya. Haki za kila mtu wa Kenya ziheshimiwe. Haki idumishwe, ufisadi umalizike Kenya.

Com. Pastor Zablon Ayonga: Asante sana. Unaweza kungoja kidogo kama Commissioner yeyote ana swali. Hakuna swali,

kitu ambacho ufanye sasa, utoe hayo maandishe kule na ujiandikishe uweke sahihi. Asante sana mzee. Next ni Titus Ndonge. Titus ninaona una memorandum? Kwa hivyo hiyo memorandum tafadhali umulike yale makubwa ambayo yaliyo katika hiyo memorandum. Unaweza kumulika utuambie yale makubwa makubwa. Na unaweza kuketi au unaweza kuongea ukisimama.

Titus Ndonge: Asante sana waheshimiwa Commissioners. Umesema naweza kuongea na kizungu kama nataka, siyo? Thank you very much. My name is Titus Theo Ndonge and I represent a group called Agape Community Initiative. I am going to present to you our memorandum, but as you said, I am just going to summarize just what we said and in connection to this, I would like to talk about two issues that we talked about because the rest are reflected in our memorandum.

I will talk about the issue first and then the suggested solution we gave. Now, the first issue is this. That brewing and drinking of traditional liquor is legal under the Traditional Legal Act, Cap. 122. However, whenever one brews this traditional liquor, especially the Kamba liquor by the name Uki, which is not harmless at all because it is made from just honey, sugar and fermented by the German Sausage fruit. Now, whenever one brews this liquor, the administration, namely Chiefs, Assistant Chiefs, and the Administration Police come and demand money, least they take you to police station. Now, that is the problem. The solution we gave is that brewing of this harmless liquor which has being sited as harmless in the various constituencies should be explicitly made legal by telling everybody so that this harassment of innocent people by the administration because of doing what their fathers and their grandfathers have being doing for long is stopped.

The law should be serious on the administrators who harass people because of drinking or brewing this liquor because like in the Kamba customary law, it is categorical imperative that this liquor should be present in matrimonial bond. When marrying, it is one of the requirement. So, that is the solution to our first problem. Should I go to our second problem or should I welcome questions from the Commissioners as you say? Thank you.

Our second problem is this. We have looked at the offices related to the Attorney General in our country and it apparently looks as though the office of the Attorney General and that of the Director of Public Prosecution are more or less the same. I will support this with quotations from our constitution.

By virtue of Section 26 (2) of the Constitution of Kenya which states as follows: 'That the Attorney General shall be the principle legal advisor to the Government of Kenya' and Section 26 (3) that 'The Attorney General shall have power to interfere with any case that he considers desirable and (a), to institute and take criminal proceedings against any person before any court other than a court martial. I will not read all this because you as learned people are well acquainted with this. You are not laymen and if I just tell you will you understand.

Now, the question is this. Under what provision in the constitution was the 1997 office of the Director of Public Prosecution established? Because if we assume that it was established under Section 24 which states that the power to establish all the

offices and that of scrapping them is vested on the President. It is assumed that this office was established under that law, then there would be an actual or apparent constitutional conflict either in letter or in conflict to use the language you understand better. The solution we suggested was this and I will also need your advice because we are lay-men. Our suggested solution was this. That this two offices should be thoroughly investigated by people who know law like yourself. If it is a duplicate, then the office of the Director of Public Prosecution should be scrapped because according to us, it doesn't look any different from that of the Attorney General. Thank you very much.

Com. Pastor Zablon Ayonga: Thank you Bwana Ndonye. You can give us your copy. Turn around to the other side. Thank you for your contribution. Next is Joseph Mulandi, or you belong to that group? Thank you so much Joseph. Mutua Munyasia? Does he belong to the group? Daniel Ngati, time is yours. You have a memorandum? Please give us some highlights. First say your names then give us the highlights.

Daniel Ngati: Thank you for the Commissioners who have given me this chance to present my views. My name is Daniel Ngao Ngati, and I have just a few views. The first one to start is on the side of the Rights of Vulnerable Groups like those disabled groups. I can say that the interest of those people who are disabled, they seem not to be taken care of. For example when there are intakes like police intakes. You find that they are not called for the interviews, whereby we are sure that if they can be called in the interviews, they can be given some work like in the offices and I think they can work in those offices in the side of the police.

The other thing I could say as a part of my views, is the side of cultural, ethnic and regional diversity and communal rights like cultural and ethnicity, I say that they should be protected and especially in our Kamba area, and also be empowered. For example, in our Kamba tribe you will find that we have things like Masia and Ngata.

Another thing as a part of views, we should have two national languages e.g. Kiswahili and English and those are just my few views I had. Thank you.

Com. Pastor Zablon Ayonga: Thank you Daniel, we have a small question for you.

Com. Kangu: Now, can you explain what Masia and Ngata means in Ukambani?

Daniel Ngati: In Ukambani, it means that it is a kind of cleansing, or it is a type of healing those superstitions according to Kamba, concerning things like witchcraft.

Com. Pastor Zablon Ayonga: Thank you. You may give your memo there and sign our register. Thank you so much. Jane Musau?

Jane Musau: Majina yangu ni Jane Mutua Musau. Niko na maoni kidogo, ile nilikuwa nataka kutoa. Ya kwanza. Sisi wanawake, tumekuwa tukinyanyaswa kidogo katika nchi hii. Kwanza tukija kwa mashamba, na properties za nyumbani. Ningependelea, tukiwa huko na Bwanagu, pahali ya mashamba, hiyo title deed tunapewa, isiandikwe yeye peke yake, tuandikwe sisi wote, Bwana na bibi. Sababu yangu, akiwa peke yake, anaenda kuuza shamba, anuzia watu wa pesa nyingi, halafu asubuhi moja anaamuka nakuta mama nikiambiwa “ondoka hii ni mali yangu”. Kwa hivyo nikiwa mmoja wao, nitaulizwa “Mama tunauza hii?” Nisema ndiyo au hapana.

Ingingine ya pili. Kama ni plot tumenunua, tuandikwe majina yetu wote, asiandikwe yeye peke yake. Sababu hii mali nimetafuta mimi na yeye. Tunaingia pahali ingine. Bwana yangu ameo mwanake mwingine, na bibi ya kwanza anakuja kuambiwa sasa wewe huyu ni mama mwenzako, muta-share hii kitu, na mimi ndiye niling’angana, kumutoa kwa mama yake, nikatafuta mali na yeye. Sasa mimi ningependelea, huyu mama mwingine akija, apate plot yake, apart from hiyo yangu niling’angana kutafuta, na waanze kutafuta na huyo Bwana, sikatai akija, sababu ni mila ya kikwetu. Asipatiwe hii mali yangu. Aende aanze kutafuta yake. Hiyo ni maoni moja.

Tena, niko naingine ile nataka kutoa. Kama Bwana yangu amefariki, imekuwa tendency ya wanawake tunafukuzwa. Ndungu zake wanasema hii mali ni yetu, mama anasema sisi hatukutaki, yule alikuwa anakujua ameondoka. Sasa mimi nafukuzwa. Ningependelea, hiyo ikuwe sheria, Bwana yangu akiaga, au akiniacha, nikae pale kwa mali ile tulitafuta na yeye, na ndungu zake ama brothers ama relatives wasikuje kuniingilia. Ikae hapo kwa hiyo mali nitunze watoto na kitu ingine yote. Hiyo ndiyo nilikuwa nayo Commissioners.

Com. Pastor Zablon Ayonga: Asante mama kwa maoni yako.

Com. Phoebe Asiyo: Mama hii katiba tunatengeneza, itakuja kukaa na nchi hii ya Kenya kwa mwiaka mingi hata kama ni miaka mia moja. Na wewe unataka tuandike kwa katiba kwamba Bwana akileta Bibi ya pili, ajengee yeye mji yake mwenye aanze mpya. Je huoni ingekuwa vizuri tukisema kwamba hakuna polygamy tena katika nchi hii? Kwa maana si ya hawa wazee. Hii ni ya wale vijukuu ambao vinakuja miaka hamsini, mia moja inakuja na ni heri kuanza kurekebisha mambo haya kwa maana wale wasichana wa miaka hizo zingine, hawatataka mtu kuja kuleta bibi mwingine kwa nyumba yake. Watakubali kweli? We unaweza kukubali na mimi naweza kukubali. Lakini wale wasichana, watakubali kuingizwa na bibi mwingine ndani ya nyumba?

Jane Musau: Nafikiri hawataweza kukubali madam Commissioner.

Com. Phoebe Asiyo: Kwa hivyo tuwafanyie mipango tu, kila mzee aoe bibi moja. Wale wameoa sasa hatuwezi kufanya kitu, lakini wale hawajaoa - -

Jane Musau: Tusema kama hiyo itawezekana, hiyo ndiyo inge kuwa best katika hii nchi yetu. Mtu akuwe tu na bibi moja.

Com. Phoebe Asiyo: Eh, hata mimi nakubaliana na wewe, maana Mungu ameumba Mtu na bibi. Ndiyo, lakini unajua wazee pengine hawatpendelea hii.

Jane Musau: Nafikiri wengi kama tribe moja moja hawatapendelea.

Com. Phoebe Asiyo: Eh, lakini tunataka kutengeneza katiba itakaa miaka mia moja, sasa tuseme wale wazee wameoa wakae namna hiyo, na wale miaka ingine inakuja - - Maana Tanzania hakuna polygamy tena. Walikataza kabisa. Na wazee wanaishi tu na wanafurahi.

Jane Musau: Hiyo ningependelea sana.

Com. Pastor Zablon Ayonga: Asante mama, lakini lazima pia nikukumbushe kwamba Waisilamu wanaruhusiwa kuwa na wanawake wanne. Na hiyo si shida yako, shida ni ile ya hawa watu wengine, Wakristo. Thank you. Anayefuata ni Mutuku Wambua. Mutuku toa maoni yako, sema majina yako na aanza.

Mutuku Wambua: Thank you Commissioners. Mine is just a statement I just want to make. My name is Richard Mutuku Wambua. I just wanted to talk about employment. Here in Kenya, we see there are so many people who are educated and those who don't have jobs. So, I want to request if in our constitution we can put that anybody who has never been employed and has attained 45 years of age, to be pensionable.

Another statement is, which I wanted to make. We live in different areas where we have different environment, different climate and if people can be helped, in the climate they suit, what can be provided there, or what can be got from the area by the government. I see this country would be moving ahead. Mine is on that, thank you.

Com. Pastor Zablon Ayonga: Asante Bwana Mutuku lakini ngoja kidogo.

Com. Kangu: Now, Bwana Mutuku, what would be your definition of employment? Kwa sababu kuna wale wako on salary employment, kuna wale wako self-employed wanafanya biashara yao, kuna wale wanalima. In terms of what you have proposed, how do we define employment ndiyo tuweze kujua who has being unemployed for 45 years?

Mutuku Wambua: Kuna watu ambao wamejaribu should I say self-employemnt? Lakini wameshindwa, sababu mahali wanakaa hakuna kitu ya kufanya and they are Kenyan citizens. Kuna wengine pia, ambao ni Wakenya na pengine walikuwa wameadhiriwa na Muhindi na amefutwa kazi halafu anakuja huku nyumbani. Hatuwezi kusema kama huyo ameadhiriwa, ndiyo

nilionelea kuwa kuna hawa watu, hawa watu wakiatain hiyo miaka arobaini na tano, wangukuwa pensionable kidogo tu.

Com. Pastor Zablon Ayonga: Una mean kidogo ni pesa ngapi?

Mutuku Wambua: Si maanishi ni pesa ngapi sababu inalingana - -

Com. Pastor Zablon Ayonga: Hapana, tunataka hiyo utuambie. Kwa maana ulipofikiria watu wakiwa miaka arobanne na mitano na wajuakuwa employed wakati wowote wapewe pension, lazima uwe umefikiria pension kama nini.

Mutuku Wambua: Ndiyo lakini unajua hii ni kitu inaendelea, na ikiendelea, miaka inasonga tu.

Com. Charles Maranga: Bwana Mutuku wacha ni kuulize. Hii group ya watu unaosema wawe pensionable, ni wale watu ambao, katika ile ili ya kimaumbile ndiyo wanatakiwa kufanya kazi kabisa. Yaani the most productive age group. Na sasa unataka kuwaambia hawa watu wakae nyumbani walipwe. Kweli serikali ya aina gani inaweza kulipa watu kama hawa wanakaa hivyo tu? Huwezi ukatoa maoni ni nini wanatakiwa wafanye? Kama sasa wewe, vile uko namna hii, you are in the age group of 30 to 45 years. Sasa wewe unataka kusema wewe uende ukae nyumbani na mzee wako ako miaka sitini na angali anafanya kazi?

Mutuku Wambua: Kuna wale wako na kazi, na wengine wamejaribu kazi wameshindwa kupata.

Com. Charles Maranga: Si ungesema pengine serikali itafute kazi ya aina mbali mbali? Kuna kazi ya kilimo, kuna kazi ya biashara, kuna kazi ya manamba, kuna kazi mingi. Si hiyo yote ni kazi?

Mutuku Wambua: na ndiyo hivyo, nimesema katika statement yangu ya pili nimesema: Mbali watu wanakaa, wasaidiwe.

Com. Hon. Phoebe Asiyo: Bwana Mutuku, nataka utuambie kwa maana hii ni katiba itakaa miaka mingi. Wewe utuambie kwamba umependekeza serikali ilete mitambo katika area hii, na maji. Hapa kuna mbuzi wengi, na kuna ngombe wengi na wakiwa na maji, munaweza kuwa na ile meat commission ijengwe hapa factory, watu hapa wafanye kazi, na wazee walio nyumbani waweke mbuzi na ngombe, walete hapa wachinjwe na wapate pesa. Lakini kusema, serikali ipeane mshahara, hiyo ni fikira kidogo, haitasaidia katiba mpya. Tuambie kile unataka serikali ifanye kwa nchi hii, watu wote wa nchi hii waweze kufaidika.

Mutuku Wambua: Hivyo ndio nilikuwa nikijaribu kusema kwa sababu kama hapa kwetu tuna maji mengi sana, hii iko hapa. Lakini unatufaidi na kitu moja tu, kuliwa na mamba, hakuna kitu ingine.

Com. Pastor Zablon Ayonga: Asante Bwana Mutuku, unaweza kwenda hapo ujiandikishe. Thank you. Tungejaribu kiasi tuwezavyo, kuongea katika lugha ambayo kila mtu ange-elewa. Si ingetusaidia? Na ninajua nyinyi kweli mtu hawezi kusema hawezi kuongea kiswahili. Kila moja wenu anaweza. Ila isipokuwa kama una shida sana, ndiyo tuende kwa mambo mengine kama Kingereza lakini uhuru ni wako. Mtu mwingine ni James Mwasia, na wakati ambao James Mwasia anakuja, nataka list ingine niletewe.

James Mwasia: Honourable Commissioners thank you very much for awarding me this opportunity. I will be as brief as possible. Mutaniwia radhi sababu nikingea kwa Kiswahili - nitajaribu lakini itakuwa kama Ki-kamba.

I would like to point the problem of the road carnage. We are losing a lot of people everyday on our Kenyan roads and as a Kenyan, I feel very much concerned and it seems as if nothing is happening. I would suggest - actually, the causes are many, like roads managed by irresponsible youth. Wale vijana wamesoma, pengine wakashindwa, mzazi akasema labdha tumpeleke awe driver, a-anze hiyo road transport. Na at the same time we have trained youth, disciplined youth in the National Youth Service. If we could get our young drivers from the National Youth Service, I hope we would minimize the road carnage.

The other thing is our roads. Not much improvement has being achieved over thirty five years after independence.

To Western Kenya. To Nakuru, Kitale by the main – I had not travelled before. The road is very narrow, catering for the whole of Western province. Very narrow, and in our new government I would think that some roads should be given first priority like roads from Nairobi to lets say Western. Kisumu and Nakuru, that road. Otherwise. It is deadly. I have had personal experience.

Again, if we will succeed in the year 2020, to be industrialized, we should prepare, our infrastructure. I also went as far as Mwingi. A place know as Mutito, Sombe. I was to be introduced as a tourist to the roads because with my big lorry, my local driver would tell me, this is the road! He could see the road but I could not see it. There was no road. So, I would highly recommend, infrastructure to be given priority.

The other thing is about poverty. Alleviation of poverty. According to me, water is the answer. Water will sum up everything, employment, what, what, what in Kenya. We have wonderful land. As a resident in Manyatta, I reside in Kithimani and I have visited National Youth Service. They are doing wonderful jobs. Big bananas, wheat. National Youth Service are producing better banana's than Kisii, Kisii country which is famous for bananas. Which means, we need water. The question of unemployment, you know, the crying , raging because our youth have no employment, the answer can be water. Water all over and God has blessed us with our good rivers. Of we give that priority, Kenya would be a wonderful country.

Before independence I was mature. I had done my O'levels. I was in Nairobi. I remember how jubilant we were that Uhuru and then when I look back after all that time, it is not good. It is a pity. We are not doing much. So, in future this

should not last forever.

On the side of education, we have excelled. Many schools work that hard and we are not lacking brain power. We have educated people. We have experts. Lets utilize them. Lets utilize them and make our country a better place.

O.K. The other thing is, my last point is about the talented students. We have 8-4-4 system. I have been a teacher, as I told you yesterday. 8-4-4 system. We don not cater for the talented students. They all go like a routine. They all go 8-4-4. I would suggest and recommend in our provinces, to have special schools for specially talented students, because they are there.

In every generation we must have akina Hilary Ngweno and the rest. So, that should be deployed otherwise we frustrate them. I would partly think some of the unruly students are not given enough work. Possibly they are very much privileged and they will finish the work and try other things. So lets monitor our privileged students and cater for them and report to the work that we can have a graduate who has gone through half the required time.

Com. Pastor Zablon Ayonga: Thank you so much.

James Mwasia: O.K. I am grateful, that was my last point. Thank you very much. Wish you every bit of luck.

Com. Pastor Zablon Ayonga: Before you go, we may want to ask you some questions.

Com. Charles Maranga: You said you are a teacher. You have said we have human resource in plenty in this country. Do you think we have excess human resource or we have adequate human resource? And then you have talked about the gifted and talented children. How do you want us to deal with that situation? Who will be responsible in identifying the gift and talented? Do you want us to start a who section of special education?

James Mwasia: Let me start with the second question. I am not suggesting you overhaul the whole system. no! Infact I am saying, we make the teachers , principle and headmasters aware so that they can pin point those children and of course I would suggest they go upto standard eight. Then from form one up to the university level, they can go to special school. From nursery to standard eight, let them all be together, but from form one, those are prileage.

Com. Maranga: You see the question I was asking, when you talk about the gifted and talented child. You can find somebody who has a unique way of seeing things. Not necessarily maybe mathematics or English or whatever. They might be other areas. You find somebody very unique. Even in parcticles, he can be very good and maybe he is not very good in other academic subjects but he is very good in pratical. Have you seen people like those ones?

James Mwasia: I am not taking of such calibre of people. Yes, I have seen that.

Com. Maranga: Now I am giving you. They are boys and girls who can for example very good in artistic whatever. They might not be good in science, they might not be good in maths, they might not be good in English, but they are very good artists. They can be u know, depict things the way you want. So, those are also talents. There are also other talents which you must know. Music, sports, and so on. So you just don't look at that narrow picture. So, I want to give you that broader sense. That they are so many people who are gifted in different things. Are you getting my point? Even sports is a gift.

James Mwasia: I understand. If I am not wrong, I think that is practiced in the U.S., if I am not wrong. Briefly, we don't have provision in Kenya. Let it be introduced.

Com. Pastor Zablun Ayonga: Now, would you like to go write a memorandum as regards to your recommendation? Write a memorandum and give it to us as regards to what Dr. Maranga and what you are planning to want to see done in this country for gifted children? You expand what your thoughts are?

James Mwasia: Is it necessary? I can do it.

Com. Pastor Zablun Ayonga: Please do. You can send to us in our office and one small question.

Com. Kangu: Bwana Mwasia, umesema road carnage kwa upande moja inaletwa by our undisciplined youth, na ukasema afadhali tuchukuwe drivers kutoka kwa National Youth Service and just before you, Mr. Ngata ametuambia there is a lot of unemployment, we should infact start paying pension to people at 45 who are unemployed. What do we do with this undisciplined youth, if we take away the jobs they have and give them to people from the Youth Service? Do we start giving them the pension that has being proposed by Ngata or what do we do with them?

Two, you have said water is the answer to our problems. But the situation in Kenya is that water, its availability or unavailability has being our biggest problem. At one point people are dying of draught. At another point people are dying of water. They are being drowned because there is too much water we don't know what to do with it, we don't know how to handle it. How do you propose that we should be able to harness this water that is going to waste and make it an answer to our problems and how do you relate that to our small scale pieces of land? Because if you embarked on giving water to all these people on their small pieces, 5, 3 acres. You cant afford. What is your programme? What would be your proposal? How do we harness the water in relation to our system of ownership of land?

James Mwasia: Thank you very much. I will start with the first question. I am not talking about the past, where mess has already being done about our irresponsible drivers. I am suggesting something to alleviate, to minimize accidents in future, and I

am not saying let us throw them away, no, no, no. The grain are still holding our cobs. I am talking about the future. To have a good percentage of our drivers from the National Youth Service and of course we can have a National system of transport marked by the State.

Com. Kangu: You are suggesting that we discipline by converting the National Youth Service into a driving school so that before they go on the roads to exercise their madness they first pass through the National Youth Service?

James Mwasia: Thank you for your question. It was the other day the Head of State who announced he would absorb 1000 graduates from National Youth Service Gilgil, and 2000 (inaudible) what about if we utilize such number for example? Let me relate this. We have Yatta, Kiharu. I come from Kithimani where Kiharu is. People in Kithimani when money is been given, they don't waste time from their small 2 acre plots to go and get free food. If we have that one Stream, why don't we continue? That was done during colonial time, way back in 1954 and after Independence we have not done much regards to water.

We have Lake Victoria, we have River Tana here, we have River Athi, we have Nyando and - - (interjections from Com. Kangu).

Com. Pastor Zablon Ayonga: Thank you so much.

James Mwasia: O.K. I am very grateful. Wish you all the best.

Com. Pastor Zablon Ayonga: Mama Ruth Kisusi? Rose unaweza kutoa majina yako, na halafu ujue una dakika tano.

Ruth Kisusi: Asante sana Bwana Mwenyekiti, majina yangu naituwa Ruth Nditho Kisusi. Natoka kwa Mwingi wa Sub Location Masinga kwa kikundi. Nataka kutoa maoni yangu kidogo. Yangu siyo mengi ni kidogo.

Kama ikiwezekana, masomo iwe ya bure bila kulipa. Na President mwenyewe wakati wa kuchaguliwa, achaguliwe na wananchi, na kura. Na akiwa ni mwanamume, makamu awe ni Mwanamke. Sisi wakina mama tunafinywa sana hata huko manyumbani mwetu. Bwana si atoe amri peke yake. Akitoa, na mimi natoa. Na wakati wa makosa, siyo niwe ni mimi peke yangu niko na makosa. Hata yeye saa ingine anashikwa na makosa. Kwa hiyo, ikiwa ni wakati wa kunipiga, labda inaweza tokea tupigane sisi wawili, na sina mengi ni hayo. Asante.

Com. Pastor Zablon Ayonga: Ikiwa akikupiga na wewe umpige?

Ruth Kisusi: Eh, kwa maana mimi ni binadamu kama yeye! Tuchapane!

Com. Pastor Zablon Ayonga: Muchapane?

Ruth Kisusi: Eh!

Com. Pastor Zablon Ayonga: Umemaliza? Huyo ni mama Ruth. Na mama kuna maswali kidogo, pengine mama mwenzako akuulize kwanza.

Com. Phoebe Asiyo: Nina swali moja tu kidogo. Unajua mama Ruth, hawa wanaume walipewe ile nguvu ile ya kinyama mingi. Yaani, siyo nguvu yaani ya kile kina wanawake, au, ile nguvu ya kinyama ile ya mwili. Wanaweza kupiga mtu mpaka waue.

Ruth Kisusi: Si wanaua kwa maana anakua anasema ameshaa peleka mali kwenu.

Com. Phoebe Asiyo: Ndiyo, na hatutaki waue watu. Sasa wewe utupe mawaidha. Kitu gani tunaweza kuandika kwa Katiba maana hatuwezi kusema watu wapigane sawa sawa, maana hapo hakuna equality. Tunaweza kusema katiba isaidiye namna gani mambo ya vita ya nyumbani, yaani domestic violence, ili kusiwe na vita nyumbani?

Ruth Kisusi: Katiba isaidie. Ikiwa ni hiyo mgogoro, tupelekane kortini. Korti iamue. Kwa maana wamezidi na kupiga sisi sana.

Com. Phoebe Asiyo: Lakini Courts haziko kila mahali. Ningependa utuambie, zamani wazee walikuwa na ile mahali yao mtu akiwa wameshindwa kuishi wanaweza kwenda wakalalamika, wazee wa kijiji wakatengeneza hiyo habari. Sasa, maana nchi ime-endelea, pengine ungetuambia tuwe na ofisi ingine, au kitu kingine kama vile watu wa Tanzania wameweka, ambayo Bwana akiwa na shida na mwanamke anaweza kwenda pale aongee, au bibi pia namna hiyo wanaita Ombudsman.

Ruth Kisusi: Kwa mila ya Kikamba tunapelekana kwa Ukoa. Ukoa wenu wanaita.

Com. Phoebe Asiyo: Inaonekana hiyo mambo ya Ukoo haijafauli Ukambani ndiyo hili ukatwambia watu wawe na equality ya kugongana.

Com. Kangu: Mama Ruth, nataka kukueleza jana kule Matuu, msichana wa shule alizungumuza na uchungu sana,

Ruth Kisusi: Kama huo niko nao.

Com. Kangu: Akisema maneno ya wazazi ya kupigana nyumbani mbele ya watoto ni mbaya, na wewe unatwambia wapigane

tu. Unafikiria nini kuhusu haki za watoto wakiangalia munatwangana kila siku?

Ruth Kisusi: Na nyinyi munezidi kutwanga sisi wakina mama. Wewe ukija ukiwa umekunywa ile “Karobo”, hata mimi nikianguka kwa miguu yako nainua mikono juu huwezi kukubali. Unaniambia niko na makosa nitakuua. Nitakuua wakati huu ujue wewe ni wangu nimekuoa. Nilipeleka mali kwenu.

Com. Pastor Zablon Ayonga: Kwa hivyo lazima mchapane? Thank you so much. Hayo ni maoni ya mama Ruth, lakini tungalipenda watu wawe na upande. Ex-Senior Chief, hakutoa jina lake lakini ametoa title. Ex-Senior Chief utoe majina yako kamili.

Simeon Munyoki : Asante sana Commissioners. Majina yangu kamili ni Ex-Senior Chief, Simeon Munyoki Kiminza. Basi maoni yangu katika nchi hii yetu ya Kenya ni taabu ya maji. Kulingana na vile tunaweza ona nchi hii ikiwa nzuri na katiba iwe inabeba kila mwananchi wa chini, tuko na mito ile inatiririka kutoka kwa milima. Kutoka kila sehemu, na tumebarikiwa kuwa na mito. Na ile serikali itakuwako miaka ishirini, miaka arobaini, miaka mia moja, hiyo mito itakuwa huko, na maoni yangu ninaona ni lazima serikali ipange mipango au ipange mipango ya kufungia hiyo mito kama Shilanga, na mvua ikinyesha, hiyo maji ikitiririka kwa hiyo Shilanga, ikiwa ni mto mkubwa iwe na dams karibu tatu. Ikijaa hii inaingia hii ingine, ikijaa hii inaingia hii ingine, na hiyo kwa maana mito ni mingi, maji haitakuwa ikimalizika na kila sehemu itakuwa na green, na kulingana na vile itakuwa mwananchi wa kawaida anaweza tumia hiyo maji kwa kulisha ngombe yake, hata pia kwa kukunywa na pia kwa kulima shamba kidogo ya mboga. Kwa hivi maoni yangu ninaona ni vizuri serikali ile itakuwako katika hii katiba tunatengeneza iwe inaangalia habari ya mito izuie kabisa maji isiwe inaenda kwa bahari.

Com. Pastor Zablon Anyonga: Point ingine.

Simeon Munyoki : Ile ingine kulingana na vile ninaona. Ile katiba tulikuwa tunafuata sana hata wakati huu ni ile ya ki-colony. Na hiyo inatengenezwa na m-colony akiwa ni na sasa ile tunataka tutengeneze kama wananchi wa Kenya ibebe mtoto, ibebe mwanamke, ni ile tunaangalia tuone ikiwa ni mtu anaoa, awe anapatana na family yake. Ikiwa ni bibi, wawe wanasema. Badala wapigane mbele ya watoto wawe wanasema kisiri kwa kikwao. Ikiwa ni mtoto waitwe wao wawili, wakutane na wasuluhishe wakiwa hapo.

Basi mtoto akiwa analemea, kuna ile mila ya ki- - ikiwa ni Mkamba ikiwa na Mkikuyu, ikiwa ni Kalenjin, ikiwa ni Mjalu, kuna watu wao wanaweza kuiita na kuzungumuza na huyu msichana au kijana au mtu mkubwa au bibi, wapange mipango ya mipangilio ya kukaa katika nyumbani.

Com. Pastor Zablon Anyonga: Thank you very much, he is Ex-Senior Chief Simeon ambaye ametupa haya mawazo na wazee hukumbuka. Thank you so much

Com. Phoebe Asiyo: (Inaudible)

Simeon Munyoki : Mimi siwezi kataa kwa maoni ya watu kwa maana wewe kama Chief unachaguliwa na watu uje uwasimamie lakini ujue mtu akiwa anachaguliwa na watu atafanya mambo ile watu wanataka kwa maana akiambiwa, ukikataa sisi hatutakuchagua tena. Kwa hivyo maoni yangu ni pawe commission ya kusimamia na kuangalia ni nani anaweza kuandikwa awe ni fit kwa hiyo kazi.

Com. Pastor Zablon Anyonga: Thank you so much Bwana Chief, unaweza kujiandikisha kule nyuma katika register. Thank you. Next, Musau J.M. J.M. Musau? Edman Thuri? Tafadhali useme majina yako kamili. Na hicho Kiswahili unaongea vizuri tafadhali? Ukisema vizuri sana unajua badala ya zile dakika nakupa tano itakuwa dakika mbili kwa maana yule anaye tafsiri atachukuwa dakika yako mbili. Hapana uchaguzi ni wako. Ukiongea Kiswahili utaongea mengi. Anza kwa majina.

Stanley Muli: Kwa jina mimi naitwa Stanley Muli na hapo niliandikwa . Hayo majina yote mbili ni yangu. Sasa, vile ambayo niliona maoni yangu, kwanza ya mbele. Ni vile ambayo niliona ile milima ambayo imekaa bila kuwekwa miti. Kama milima ingewekwa miti, ingekuwa mzuri shauri ya hewa.

Ya pili, ni vile ambayo niliona, kama ni Headman kama mimi. Headman ni mtu ambaye ni wa chini kabisa. Na ni mtu ambaye anajulikana kabisa. Kwa hiyo, kama ni Headman, lazima apewe pesa maanake ndiye mtu yule wa chini kabisa na ndiyo anamaoni ya watu wale ambaye anasimamia.

Ya tatu. Kama hii katiba mzuri. Katiba lazima ijengwe ni mtu akiwa ni mtu ambaye amesema kama vile mimi nimesema. Ili tuwe na mawasiliano vizuri. tuwe ni mtu ambaye anaona yule mwingini kama rafiki yake, na huo ni ukoo wangu. Si mtu ambaye alionekana akiwa ana wivu ndani ya mtu. Uwe ni mtu ambaye unaona, hawa watu wote waliletwa huko ni Mungu, ni watu wa kueleanwa. Sasa kwa hiyo, sijui hapo itakuwa namna gani.

Com. Pastor Zablon Anyonga: Asante Bwana Headman. Kuna jingine?

Stanley Muli: Kile kingine naweza kutaja kidogo ni ukame ule ambao uko hapa Masinga. Masinga hii tuna taabu ya maji kabisa, na kama maji ingewekwa ikiwa ni ya kuzunguka. Ikiwa inawekwa kama kuna mto ambaye anaitwa Tulimumba. Hiyo tulimumbu kama inge pigiwa koo, maji inaweza kuonekana vizuri. kuna mtu mwingine anaitwa Ngila. Na hiyo Ngila kama ingewekwa koo vile vile. Maji itakuwa ni mingi kwetu. Kwa hiyo mambo yangu ni hayo.

Com. Pastor Zablon Anyonga: Hamuna swali enda hap nyuma ujiandikishe hapo. Na kuna Headman mwingine, Dhamburi. J.K. Mutua? Kama J.K. hayuko. Julius Mutuku? Na Pius Gitonga? Pius unaonekana una memo. Utupe maoni makubwa

makubwa kwa maana hiyo tutaenda kusoma usitusomee hapa, na kwa hiyo toa majina yako.

Pius Gitonga: O.K. Mimi naitwa Pius Gitonga. Yangu ni machache. Secondary schools and primary schools education free. Hawa walimu wa nursery wapatiwe mshahara kutoka (inaudible) waandikwe na serikali. NSSF ilipe wa-member wao kutokana na wakati waliacha kazi, lakini hii kama ile miaka yao wanasema, almost 55 years. Kwa sababu hiyo ni haki ya mtu, na akiwacha kazi anaweza kulipwa hiyo pesa yake. Aende ajisaidie mahali.

Hawa Headmen, wapatiwe mshahara na serikali. Chiefs, Assistant Chiefs, waende transfer kama wafanyi kazi wale wengine. Na wawe wakifanyiwa selection na raia, wananchi. Hii County Council ya Machakos au in general county council for example County Council ya Machakos, inatoa hii wanaita penalty. Wakati wa mwezi wa tisa imeisha. Kwa wale watu wanafanya biashara. County Council ya Machakos, inatoa hii wanaita penalty, wakati ya mwezi wa sita umeisha kwa wanabiashara.

Com. Pastor Zablon Anyonga: Kwa hiyo unataka wafanyeje? Watoe mwezi wa saba?

Stanley Muli: Wafanye collection ya license peke yake, bila kutoa hii penalty. Ni ya nini? Hii County Council ya Machakos, inaweza kuachana na hii rent ya kulipisha maduka wale walijenga na ambao hawana kazi ndani yake. Hii ni plain, to one third, wanalipisha rent lakini hakuna kazi inaendelea hapa. Walipishe rent kwa ile duka inaendelea na biashara. Thank you.

Com. Pastor Zablon Anyonga: Thank you so much. Any questions? Thank you, unaweza kutuachia hayo maandishi hapa na uweke sahini. Raphael Mutua? Now, Mulwa Wambua? Mulwa Wambua get ready na uchukuwe hiyo toa majina yako.

Mulwa Wambua: Mimi naitwa Mulwa Wambua, hasa mimi ni mkaaji wa hapa hapa Masinga. Langu ni kidogo ningetaka kugusia ni kwamba, sisi watu wa Masinga tuna maji ambaye tunaye karibu hapa kwenye dam. Na ile dam yenyewe, ile maji yenyewe haitusaidii sisi tabu tunaye nyingi sana, na ingawa tuna uwezo wa kufanya kazi. Isipokuwa hatuwezi yale maji kuyatoa kule kwenye dam kuyaleta pande hii, kwa hivyo tunge-uliza ikiwezekana serikali itusaidie kuyatoa yale maji kule kwenye dam, kuyasambaza sehemu ya Masinga. Serikali inaweza ikatupa hata kama ni loan, watuwekee maji halafu tutaachwa tukilipa baadaye, ndiyo tuweze kufaidika. Unajua kazi yenyewe inakosa, siku hizi hakuna kazi. Lakini serikali ikitusaidia kwa njia hiyo tunaweza tukajimudu sisi. Kwa hivyo yangu ni hayo hayo.

Com. Pastor Zablon Anyonga: Thank you so much. Hebu jiandikishe kule nyuma. Nicholas Muhonzi? Anaye fuata atakuwa ni Anna Ndinda, na atakaye mfuata Anna atakuwa Abraham Ngatu. Endelea, toa majina yako na endelea.

Nicholas Wambua: Asante sana Commissioners. Majina yangu kamili naitwa Nicholas Wambua Ngozi. Na washukuru nyinyi nyote waliohudhuria kikao hichi. Ningependa kuongea kwa Kingereza kama itawezekana.

First I will talk about individual recognition, vis-a-vis the right to life and that entails; first abortion and contraceptions. We know that truth has no democracy. You cannot line up and you know, you fought for truth. Truth you know always is absolute and it is a common currency that life is sacred and it is a gift from God and no one has a right to take it away. So I don't know the fuss about the government legislating what God has ordained. They are divine laws, so we should not be involved in discussions about whether we are supposed to legalize abortions, contraception and pills. For my own view, I would say that that is a divine law and it is period – there is no question about it and I don't even understand why the government can propose or recommend to buy condoms, and people are suffering. They have no food to eat, they have no basic rights as such.

Com. Pastor Zablon Anyonga: Give us your recommendations Bwana Nicholas.

Nicholas Wambua: My recommendation is that in the constitution we are supposed to be involved all of us, there should not be any clause whatsoever, about you know, abortion and contraception's. Simple. Next I will talk about multi-roles or duplications of jobs. Occupancy of many offices which sometimes leads to inefficiency. If I am to give a solid example, I don't know - -all my life there is a lady, I would presume is Phoebe Asiyu, I don't know her, but I would like to relate with her and feel you know - that touchy feeling because really I should be knowing her and also the other members of the commission. So, in this point of multi-roles, you may find that she may be occupying so many offices, doing so many roles and they are other people who are also qualified. So, this duplicating of roles and jobs. So, I mean equity, fairness in distribution of whatever we have in the country.

